LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# MATUNZO YA MTOTO

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp
ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

# MATUNZO YA MTOTO

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


SHUKRANI ........................................................................................5
DIBAJI ...............................................................................................5
UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU......................................................................................7
MAONO ..............................................................................................8
TAMKO LA LENGO MAHUSUSI .......................................................8
LENGO KUU ......................................................................................8
Utangulizi...........................................................................................9
Nani anaweza kupeleka maombi ya matunzo ya mtoto . 10
Nani Anaweza Kushitakiwa Kwa Matunzo Ya Mtoto........11
Mahakama ipi yenye uwezo kisheria kusikiliza maombi ya matunzo ya mtoto ..........................................................11
Vitu vya kuzingatia kabla ya kutoa amri ya matunzo ya mtoto. ...................................................................................... 12
Malipo ya matunzo ya mtoto yanaweza kulipwa kwa nani? ...................................................................................16
Utekelezaji wa amri ya matunzo ya mtoto ............................17
Mabadiliko katika amri ya matunzo ya mtoto....................18
Hitimisho.........................................................................................19

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani za dhati kwa mwanasheria wetu Wakili Hamisi Mayombo pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu hususani ofisi ya Arusha kwa kukiandaa kijitabu hiki.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote

kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.

Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako upata usaidizi huu.
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.**

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo yapo Dar es Salaam. Pia Kituo kina ofisi nyingine Arusha na Dodoma.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

## Utangulizi.

Katika migogoro mingi ya ndoa, au inayohusiana na ndoa watoto wamekuwa waathirika wakubwa pale ndoa hiyo inapovunjika au wazazi wanapotengana. Mara nyingi wanawake wamekuwa wakiachiwa mzigo wa kuwatunza watoto bila ya kupata usaidizi wowote kutoka kwa baba. Lakini watu wengi hasa wanawake wamekuwa hawafahamu hatua zipi wachukue, au wapi waende ili waweze kupata matunzo ya mtoto kutoka kwa mzazi mwenzie. Hivyo basi kijarida hiki kimekusudia kueleza kwa lugha nyepesi taratibu za kufuata pale inapotokea mzazi mmoja au wote au mtu mwenye wajibu wa kutoa matunzo ya mtoto ameshindwa kutekeleza wajibu wake kisheria wa kutoa matunzo ya watoto.

## Nani anaweza kupeleka maombi ya matunzo ya mtoto

Kwa mujibu ya sheria ya mtoto ya mwaka 2009, watu wafuataao wanaweza kupeleka maombi ya matunzo ya mtoto katika mahakama. Watu hao ni kama ifuatavyo;

i. Mtoto kupitia msimamizi wake,
ii. Afisa ustawi wa jamii,
iii. Askari wa polisi,
iv. Mzazi,
v. Mlezi
vi. Ndugu wa mtoto,
vii. Kwa kibali maalum cha mahakama mtu mwingine yeyote.

Vilevile lazima ikumbukwe kuwa maombi ya matunzo ya mtoto yanapelekwa katika mahakama ya watoto (Juvenile Court) ambazo zinapatikana kwenye kila mahakama za wilaya na au Mahakama za Hakimu Mkazi nchini au Mahakama zingine zozote zitakazo tangazwa na Jaji Mkuu kadiri atakavyoona inafaa.

## Nani Anaweza Kushitakiwa Kwa Matunzo Ya Mtoto

Maombi ya matunzo ya mtoto yanaweza kufunguliwa dhidi ya mzazi mmoja au wote wawili kutegemeana na mazingira ya shauri. Vilevile shauri la matunzo ya mtoto linaweza kufunguliwa dhidi ya mtu mwingine yoyote ambaye ana wajibu wa kumlea au kumtunza mtoto husika. Hivyo kwenye suala la matunzo ya mtoto si lazima wazazi tu ndiyo wanaoweza kushitakiwa hata mtu mwingine anaweza kushtakiwa endapo sheria itamtambua kuwa ndiye mwenye jukumu la kutoa matunzo ya mtoto.

## Mahakama ipi yenye uwezo kisheria kusikiliza maombi ya matunzo ya mtoto

Kwa mujibu wa sheria ya mtoto ya mwaka 2009 maombi ya matunzo ya mtoto yanatakiwa kufunguliwa katika mahakama ya watoto.

Mahakama hizo za watoto zinapatikana katika majengo ya mahakama za wilaya na mahakama za hakimu mkazi na mahakama zingine, kadiri Jaji Mkuu atakavyoona inafaa. Mahakimu wenye uwezo kisheria wa kusikiliza maombi ya matunzo ya mtoto ni mahakimu wakazi.

## Vitu vya kuzingatia kabla ya kutoa amri ya matunzo ya mtoto.

Katika kutoa amri ya matunzo ya mtoto kwa mzazi au mtu ambaye anawajibu kisheria kumtunza mtoto mahakama itazingatia kipato cha mhusika. Hivyo mahakama itazingatia mambo yafuatayo kabla haijatoa amri ya matunzo ya mtoto;

- Mshahara, ujira, faida inayopatikana kutokana na biashara au kazi fulani, bonasi na posho ambayo mzazi au mtu mwenye wajibu wa kutoa matunzo ya mtoto anapata katika shughuli zake. Hivyo

mahakama inalazimika kutoa amri ya matunzo ya mtoto kwa kuzingatia vipato hivyo hapo juu.

- Huduma zilizowahi kutolewa kwa mtoto na mhusika hapo kabla.
- Shughuli za kibiashara za mzazi au mtu mwenye wajibu wa kutoa matunzo ya mtoto. Mahakama itatakiwa kuzingatia aina ya biashara na faida anayoipata mzazi au mtu mwenye wajibu wa kumtunza mtoto.
- Mafao au kiinua mgongo ambacho mzazi au mtu anayewajibika kutoa matunzo ya mtoto analipwa au atakacholipwa. Hii hutokea pale ambapo mzazi au mtu anayewajibika kumtunza mtoto amestaafu au mkataba wa ajira umefika mwisho au kusitishwa. Hivyo mahakama inawajibika kuzingatia kiasi cha fedha atakacholipwa au anacholipwa muhusika kabla ya kutoa amri ya matunzo.
- Gawio au riba anayoipata mzazi au mtu ambaye ana wajibu wa kumlea mtoto.

Tunaposema gawio hii ina maana kiasi cha fedha au faida mtu anayoipata baada ya kuwekeza katika kampuni au shirika fulani ambapo hulipwa kila baada ya muda fulani. Na riba ni ongezeko la fedha mtu analolipata kutokana na kuweka fedha zake, inaweza kuwa benki au taasisi yoyote ile. Hivyo kwenye kutoa amri ya matunzo mahakama itazingitia kiasi anachokipata mzazi au mtu mwenye wajibu wa kutoa matunzo ya mtoto.

- Faida anayoipata mzazi au mtu ambaye ana wajibu wa kumlea mtoto kutokana na kodi ya nyumba, kilimo, mifugo na shughuli nyingine zinazoendana na hizo.
- Mahitaji ya wategemezi wengine ambao mzazi au mtu mwenye wajibu wa kumtunza mtoto husika anawajibika kutoa matunzo. Wakati mwingine mzazi au mtu mwenye wajibu wa kutoa matunzo kwa mtoto anaweza kuwa na kipato kikubwa lakini kuna wategemezi wengine wako nyuma yake. Hivyo mahakama kabla haijatoa

amri ya matunzo ya mtoto itahitajika kuzingatia majukumu aliyonayo mzazi au mtu mwenye jukumu la kutoa matunzo ya mtoto kwa wategemezi wengine.

Ili mahakama iweze kujiridhisha yenyewe na taarifa za kipato ilizonazo kuhusiana na mzazi au mtu mwenye wajibu wa kumlea mtoto inaweza kumuomba afisa ustawi wa jamii wa sehemu husika kuandaa taarifa ya uchunguzi kuhusiana na;

i. Uwezo wa mzazi au mtu mwingine katika kumtunza na kumlea mtoto.
ii. Kujiridhisha na ukweli wa maelezo yoyote yaliyotolewa kuhusiana na kipato, matumizi na majukumu ya mzazi au mtu yoyote anayewajibika kumtunza mtoto.

Lakini afisa ustawi wa jamii kabla ya kuanza kufanya uchunguzi sheria inamhitaji kutoa taarifa (notisi) kwa mzazi asiyeishi na mtoto, mtu anayeishi na mtoto  na waajiri wa wazazi wote wawili kama wapo. Vilevile sheria

inamtaka afisa ustawi wa jamii kuwasilisha taarifa yake ya uchunguzi mahakamani ndani ya siku kumi na nne (14) toka siku ambayo amri imetolewa.

## Malipo ya matunzo ya mtoto yanaweza kulipwa kwa nani?

Sheria inaitaka mahakama ya watoto kutoa amri ya malipo ya matunzo ya mtoto kwa kupitia watu wafuatao

- Mzazi au mtu yoyote anayeishi na mtoto
- Mkuu wa idara ya ustawi wa jamii.
- Au mtu yoyote ambaye mahakama itaona inafaa kwa vipindi tofauti tofauti.

Mahakama vilevile inaweza kutoa amri ya malipo hayo ya matunzo kwa mtoto kutolewa katika muda tofauti tofauti kadiri mazingira yatakavyokuwa. Mahakama pia kila mwaka inaweza kubadili au kupitia amri ya malipo ya matunzo kwa mtoto kwa lengo la kuhakikisha

amri husika inatekelezwa, mabadiliko ya makazi na mabadiliko ya ajira au biashara na mambo mengine kadiri mazingira yatakavyokuwa yanaonesha.

## Utekelezaji wa amri ya matunzo ya mtoto

Kama itatokea mzazi au mtu mwenye jukumu la kumtunza mtoto hajatekeleza amri ya matunzo kwa muda wa siku ishirini na nane (28) toka siku ambayo imetolewa, basi maombi ya utekelezaji wa amri hiyo yataombwa mahakamani dhidi ya mzazi au mtu yoyote ambaye amri inamtaka atekeleze amri hiyo. Lakini kabla ya kupeleka maombi hayo ya utekelezaji wa hukumu muhusika/mwombaji atahitajika kupeleka notisi ya kumtaka mzazi atakeleze amri hiyo ya mahakama.

Katika shauri la matunzo ya mtoto kama mahakama ilipitisha amri ya malipo ya fedha

basi utekelezaji utafanyika kama utekelezwaji mwingine unaofanyika katika mashauri mengine ya madai kwa mujibu wa kanuni za utaratibu wa mashauri ya madai.

## Mabadiliko katika amri ya matunzo ya mtoto

Mzazi au mtu yoyote ambaye ana jukumu la uangalizi wa mtoto au ambaye anawajibika kutoa matunzo ya mtoto anaweza kupeleka maombi mahakamani ya kubadilisha amri ya matunzo ya mtoto kulingana na mazingira yaliyopo. Kabla mahakama haijabadilisha amri ya matunzo ya mtoto itahitajika kuzingatia mambo yafuatayo;

- Mabadiliko ya msingi na kimaisha toka siku ambayo amri husika imetolewa
- Matakwa ya kimsingi ya mtoto.
- Uwezo wa mzazi kulipa gharama za matunzo.

## Hitimisho

Msomaji wa kijarida hiki lazima ufahamu kuwa chochote kinachofanyika kisheria juu ya mtoto lazima kifanyike na kizingatie matakwa na maslahi ya msingi ya mtoto husika. Hivyo tafsiri ya sheria au uendeshaji wa mashauri yanayohusiana na mtoto ni lazima yafanyike kwa kuzingatia maslahi mapana ya mtoto. Hivyo tafsiri yoyote itakayotolewa na mahakama au chombo chochote na kuonekana kuwa inamkandamiza mtoto basi tafsiri hiyo itakuwa batili na kinyume cha sheria.

Sweden Sverige

Norwegian Embassy

FORD FOUNDATION

Irish Aid
Rialtas na hÉireann
Government of Ireland

Ministry for Foreign Affairs of Finland


**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (MAKAO MAKUU)**
Jengo la Jaji Lugakingira,
S. L. P. 75254, Kijitonyama, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz
**Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA**
Mtaa wa Isere - Kinondoni, S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA**
Barabara ya Olerian, Olosiva, Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Idd,
S. L. P. 15243, Arusha – Tanzania **Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu na 22. Area D, S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz    HakiTV